***„Yesu Kristo ni yeye yule, jana leo na hata milele“***

(Waebrania 13:8)

# BARUA YA MZUNGUKO SEPTEMBA 1972

Nina wasaalimu kwa moyo wangu wote ndani ya jina la thamani la Yesu, kwa maana haya ya lsaya 54:14, 15, 17:

*“Utathibitika katika haki. Utakuwa mbali na kuonewa, kwa maneno hutaogopa, na mbali na hofu, kwa maana haita kukaribia tazama, yamkini watakusanyana, lakini si kwa shauri langu. Watu wo wote watakao kusanyana juu yako wataaguka kwa ajili yako. Kila silaha itakayofanyika juu yako haitafanikiwa, na kila ulimi utakao inuka juu yako katika hukumu utauhukumiwa kuwa mkosa. Huu ndiyo urithi wa watumishi wa BWANA na haki yao inayotoka kwangu mimi, Asema BWANA”.*

Tunapashwa kuwa na uhakika wa hii, ya kwamba Mungu anapigana kwa ajili yetu, kama tunasimama kwa upande wake. Tuna jikuta katikati ya vita vya kiroho; lakini BWANA amekwisha kushinda nguvu zote za yule adui. Hatupashwi wala kuogopa, wala kuwa na hofu kinyume ya ile tukiwa wenye kujawa na uhakika mwingi tunasema: *“Kama Mungu yuko kwa upande wetu, ni nani atakaye kuwa juu yetu? Watu wanaweza kutufanya nini?.”* Hakuna silaha hata moja iliyo fanyika juu ya watu wa Mungu itakayo fanikiwa kuwa gusa, na kila ulimi utatao jiinua juu ya wateule utahakikishwa kuwa ni wauwongo. Huu ndiyo urithi wa yule amwaminiye Mungu kwa moyo wote na anaye mtumainia yeye.

## HABARI ZA SAFARI YA UTUME

Katika miezi iliopita, nilipata upya wakati wakuona namna gani Mungu anapatia inchi nyingi uamsho: lwe huko Finlande, ao huko sicile, huko ulaya ao katika bara zingine, pahali pote watu wana shuhudia. Kwamba kwa neno la Mungu lilo funuliwa wali pokea chakula cha kiroho walicho kuwa wakikingojea tangu siku nyingi. Mahubiri ya ndugu Branham ya metawanyika katika lugha mbali mbali, katika umbo za kanda na za vitabu. Mungu anakesha ili Neno lake lisirudie bure kwake, na analifunulia walio wake kwa Roho Mtakatifu. Kweli ya Biblia zinatoa miale ya nuru timilifu ya Mungu, kuliko vile haijawahi kuwako hapo mbele. Igawa, hatuna

nafasi ili kuonyesha kimoja kwa kimoja kile ambacho Mungu anachokifanya kwa hesabu kubwa kama hiyo ya watu.

## MASWALI NA MAJIBU

Miezi hii iliyopita, BWANA alionioyesha umuhimu wakuonyesha, kwenye nuru ya maandiko, misingi kwa ajili ya ujengaji wa lile Kanisa. Miongoni mwa wandugu, mara kwa mara inaulizwa: "Namna gani mutu anaweza kujua kama ameitwa kuhubiri na mapashwa yake ni gani ndani Ya ufalme wa Mungu. wazee wanawekwa namna gani na wanapashwa kutimiza shurti gani?

Kwa makusudi mpaka sasa sija zungumzia maswali haya kwa sababu nilipokea tu toka kwa BWANA kazi ya kwenda muji kwa muji ili kutangaza humo Neno lililo funuliwa. Si kupokea agizo la kuanzisha Makanisa wala kuweka wazee. Nina hisia ya kwamba hamtatokea kanuni mpya za imani ndani ya huu utangazaji wa Neno ulio wa mwisho na ambao nyuma yake hakuna mwengine unao fanana nao, bali mwili wa Yesu Kristo, katika ujumla wake, ule ambao utanyakuliwa. Bali kwa kuangalia makanisa yaliyoko, siwezi kujindoa kwenye wajibu wa kutangaza shauri zote za Mungu: Agizo kwa ajili ya ujengaji wa kanisa ni sehemu yake nani mapashwa kwangu mimi kuonyesha namna gani huduma mbali mbali ziko ndani ya kazi katika Kanisa.

## KANISA LA YESU KRISTO

Kanisa la Yesu Kristo siyo matengenezo ya kiutu, bali ni uumbaji wa Mungu. Kristo alisema: *"Nami na kwambia… kwamba juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu, na milango yakuzimu haitalishinda."* Kuzaliwa na kuudwa kwa Kanisa la Yesu-kristo vinatokana na tendo la Mungu. Kanisa lake linawekwa peke yake chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu na wa Neno la Mungu. Matafisri na kanuni za watu hazina nafasi hata moja ndani yake. Kielelezo tu mekipewa ndani ya uundaji na ujengaji wa lile Kanisa la kwanza la ki Kristo, kama vile tunavyo elezewa ile ndani ya maandiko.

Tunataka zaidi sana kwa namna ya kipekee kuonyesha zile huduma tano na kuwekwa kwa wazee, ili kuonyesha namna gani hawa wanatumika ndani ya Kanisa. Kulingana na Waefeso 4:11-12, Mungu aliweka Mitume, Manabii, Wainjilisti, Wachungaji na Waalimu. Hizi

huduma tano zime wekewa kwa kuujenga mwili wa Kristo na kwa kuongoza watakatifu kuwa wenye uwezo katika utenaji wa kazi ya Kanisa. Pale ambapo hizi huduma tano zina kosa, haiwezi hata kusemeka kuhusu utendaji wa kazi hii, wala juu ujengaji wa mwili wa Kristo, Mungu ametoa hizi huduma tano kwa ujumla ya Kanisa, na ndiyo maana inafaa mwito wa kiungu kwa kuitenda. Hakuna hata mtume mmoja, nabii, muinjilisti, mchungaji ao mwalimu anayeweza kuitwa ao kuchanguliwa na Kanisa, kinyume yake imeandikwa vema: *"Naye alitoa wamoja…"*

Ndani ya Kanisa la Agano jipya, tuna pata kwanza kazi ya mitume, kwa maana BWANA aliwapatia siri za Neno lake. Yote yaliyofunuliwa manabii wa Agano la kale katika yale yanayohusu mpango ya wokovu, tunayaona yakitimilika katika nyakati za Kanisa la Agano jipya. Mitume walikuwa na namna moja ya kuona ya kipekee inayopenya ya kazi ya wokovu wa Mungu, na walipokea toka kwake kazi ya kutangazia Kanisa ile ambayo BWANA aliwapa. Paulo alishika kwa thamani kubwa huduma yake ya mtume, kwa ginsi alijionyesha kila mara kwa namna hiyo kwenye mwanzo wa barua zake. Aliwaandikia Warumi:

*"Paulo mtumishi wa Yesu Kristo, aliyeitwa kuwa mtume, aliyetengwa aihubiri injili ya Mungu; ambayo Mungu amekwisha kuiahidi kwa kinywa cha manabii wake katika maandiko matakatifu…"*

Katika 1 Wakorintho 1, anasema: *"Paulo aliyeitwa kuwa mtume wa Yesu Kristo kwa mapenzi ya Mungu…"*

Ndani ya 2 Wakorintho 1, Wagalatia 1, na Wakolossai 1, yameandikwa karibu maneno mmoja. Ndani ya Tito1 anasema:

*"Paulo, mtume wa wangu, na mtume wa Yesu Kristo, kwa ajili ya imani ya wateule wa Mungu, na ujuzi wa kweli ile iletayo utauwa".* Inaonekana toka maneno hayo ya kwamba Paulo hakuwa na tia mkazo juu ya kazi ya uinjilisti, bali juu ya uwajibu wake kulingana na imani ya wateule wa Mungu na ujuzi wa kweli. Kama leo mtumishi mmoja wa Mungu angejionyesha mwanzo wa mahubiri yake kama alivyo fanya Paulo, tungelizania kuwa hayuko kwenye nafasi yake. Bali Paulo, aliishika kua yenye kustahili, akiongozwa na Roho wa Mungu, kusema tangu mwanzo wa barua zake huduma yake ilikua gani ambayo Mungu alimkabidhi uzito gani. Mambo haya yanaonyesha kwamba akiwa mtu wa Mungu alisimamia na kueleza oni la kiungu. Kile ambacho alikua akifafanua kuhusu mpango ya

wokuvu kutokana na ono la unabiii likua pia yenyi kushurtishwa kama yale manfundisho aliyo kuwa akiyaandika. Maagizo kwa ajili ya Kanisa kuhusu Ubatizo, Meza ya BWANA, utendaji wa karama za Roho ao kuwekwa kwa Wazee ndani ya kanisa la mahali, alivifunuliwa na Mungu.

## NI NANI ALIYE NA SEHEMU KWA UJENGAJI WA KANISA?

1 Wakorintho 12:4-11 inatuonyesha tendo mbali mbali la Roho Mtakatifu ndani ya kila kiungo cha Kanisa la Yesu Kristo. Kwa namna ilio wazi Neno hili liko kama kiyoo ambamo tuna weza kujiangalia kwa ajili ya kuona ni wapi lipo. Tuna soma kwenye shahili la 7: *"Lakini kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa kufaidiana"*.

Kila mtoto wa Mungu atashikwa na tendo la Roho mtakatifu, na kwa wote ufunua Roho utapewa kwa kufaidiana, tangu shahili la 8, zile zihirisho kenda za Roho Mtakatifu, tunazionyeshwa ginsi zina jitandaza kwa ufunuo wa karama kenda za Roho. Kwenye shahili ya 11, imesemeka: *"Lakini kazi zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye Yule, akimgawiya kila mtu peke yake kama apendavyo yeye"*. Basi ni ushuhuda wa biblia kwamba kila mmoja wa wale walio wa Kanisa la yesu kristo anayo sehemu kwenye tendo la Roho Mtakatifu.

## KANISA LA KWELI KAMA VILE MWILI WA KRISTO

Katika 1 Wakorintho 12:12, Kanisa linaonyeshwa kama mwili wa kiroho ambao unaundwa na viungo vingi. Viungo vya mwili viko tafauti; bali vinakua kila kimoja ni kiungo cha mwezake kimoja kwa kingine, vikiambatana vimoja kwa vingine na vinaungana kwa ngozi ambayo inavifunika. Mwili mzima wa yesu kristo unazunguka zungukwa na uzima wa kristo, na unavikwa na nguvu yake. Ku shahiri ya 13 imesemeka, tumebatizwa wote ndani ya Roho mmoja na wote kwamba tume nywesha kwa Roho mmoja. Hiyo ndio ushuhuda wa maandiko matakatifu. Kila mwamini wa kweli amebatizwa kwa Roho Mtakatifu ndani ya Kanisa la Mungu aliye hai na kwa hiyo amewekwa chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu. Licha ya tofauti zao viungo vyote vya mwili wa Yesu Kristo vitaheshimianina vitatambuana, kwa maana pomoja, vinaunda mwili mmoja navinamtiii Kristo, ambaye ni kichwa.

## MUNGU ALIWEKA

Tunasoma katika 1 Wakorintho 12:28: *"Na Mungu ameweka wengine katika Kanisa, wakwanza Mitume, wapili Manabii, watatu Waalimu…"* Basi tunaona kwamba kusanyiko haliundwe na watu, bali na Yesu Kristo tunatambua pia ya kwamba yote inayojiita Kanisa la BWANA haliko Kanisa tu kwa sababu hiyo maelezo haya ya kibiblia ya metolewa ili kumusaidia kila mmoja kwa kujihoji mwenyewe, ili kuona kama ni wa kwamba Mungu ameweka ndani ya Kanisa: *"Kwanza Mitume, pili Manabii, watatu Waalimu na kadhalika…"*

Wote ambao nisehemu ya Kanisa la Yesu Kristo wana heshimu utaratibu wa kiungu na wanatambua huduma ya mtumishi aliye tumwa na Mungu, iweni ile ya mtume, ya nabii ao ya mwalimu. Yote ambayo Mungu aliyo weka kwa ujenzi wa Kanisa, wale ambao wanao kua sehemu ya mwili wa Kristo wanaichukua na shukrani. Kwa kawaida watu, wanatambua huduma ya muchungaji ao ya muinjilisti, bali ya nayo husu zile tatu zingine ile inaonekana kuwa ni tofauti sana. Lakini Mungu aliamua ya kwamba hizi zilikua za lazima na aliziwekea ujenzi wa Kanisa.

Tunasoma ndani ya Matendo 13:1: *"Na huko Antiokia katika Kanisa lililo kuwako palikuwa na manabii na waalimu……"* kiisha ma jina ya watumishi hawa tunayapewa. Wakati walipo kuwa wakimtumikia BWANA katika huduma zao, Roho Mtakatifu akasema:

*"Nitengeeni Barnaba na Sauli kwa ile kazi niliyowaitia"*. Tambueni kwamba wali waongoosheya mikono, kama alama ya kuwasindikiza na siyo kwa ajili ya kuwa weka katika huduma yao, kwa maana kulikuwa muda murefu ambamo hii ilikuwa imekwisha kuthibitishwa na Mungu. Kwenye shahiri 4 imesemwa: *"Barnaba na Sauli walio tumwa na Roho Mtakatifu…"*

Ni ile ndiyo tunayo hitaji leo. Watu wa Mungu ambao mwito na huduma viwe vimefunuliwa na ku thibitishwa ndani ya kusanyiko mbele waweze kwanda zao.

Leo, tunasikia mara kwa mara watu wakisema: "Tunaye Kristo na ndiyo sababu hatuitaji wala mitume, wala manabii". Je kwa hayo wanataka kusema ya kwamba Kanisa la pale mwanzo hali kuwa naye kristo na ndiyo sababu mungu aliweka mitume, Manabii, na Waalimu na ndivyo hivi? Wanataka kusema ya kwamba Kanisa la Antiokia **halikukuwa** naye Kristo, kwa sababu kule manabii na waalimu walitimiza huduma yao chini ya uogozi wa Roho mtakati-

fu? Ni kinyume cha yale, ndiyo kweli. Kila Kanisa ambalo litakuwa kweli kweli na Yesu Kristo litakuwa pia na kazi ya huduma ndani yake.

Kazi ya Mtume ina sehemu kubwa kwa kuenda katika shamba la utume, siyo tu kwa ajili ya kuihubiri injili kule, kama ilivyo kwa wainjilisti, bali kwa kubakia pahali pamoja mpaka kanisa lizaliwe na kwamba wazee waweze kuwekwa pale. Kazi ya Nabii wa Kanisa la Agano jipya kuwekawazi ao kueleza Neno la Kinabii, kulingana na maana yake ya kiungu. Katika 1 Wakorinto 14:29, Paulo anaandika:

*"Na manabii wanene walili ao watatu, na wengine wapambanue, lakini mwengine aliye keti akifunuliwa Neno, Yule wa kwanza anyamaze. Kwa maana ninyi nyote mwaweza kuhutubu mmoja, ili wote wapate kujifunza na wote wafarijiwe. Na Roho za nabii huwatii manabii".*

Kwa nini Biblia ingetoa habari kama hii, kama Mungu hangelikuwa na nia ya kuongoza katika matendo watu wake kupitia zile huduma za kinabii? Ni wazi ya kwamba hapa haihusu zawadi ya unabii. Tunaiona kwa jumla ya mawazo yanayo kuwa ndani, kwa maana imeandikwa: *"Lakini mwengine aliye keti akifunuliwa Neno, Yule wa kwanza na anyamaze."* Bali kamwe, unabii unapotolewa, mutu hawezi kunyamazishwa. Unabii ni Neno linalotoka moja kwa moja kwa Mungu, kwa upuiziyo wa Roho Mtakatifu.

Paulo anasema kwenye shahiri ya 6: *"… Nitawafaidia nini, isipokuwa nasema nanyi kwanjia ya ufunuo, ao kwa njia ya elimu, ao kwa njia ya unabii ao kwa njia ya mafundisho?"*

Wengi wananzania nabii kama mwenye kutangulia tu kusema mambo yatakayo kuja pekee, ao anayefunuwa vitu vilivyo sasa mbavyo vinahusu Kanisa. Bali, kazi ya kinabii inajifunua ndani ya Agano jipya kwa namna mbali mbali; kwa namna ya kipekee katika kulitangaza Neno kwa Kanisa, chini ya uongozi na kwa ufunuo wa Roho Mtakatifu kwa namna iliyo sahihi. Mara kwa mara zinakutwa, zikiungana sana, kazi ya Mtume, ile ya Nabii, na ile ya Mwalimu.

Katika 2 Timotheo 1:11, Paulo anaandika: *"…Naliwekwa niwe muhubiri, na mtume na mwalimu wa mataifa".* Kwenye shahiri ya 13, anasema: *"Shika kielelezo cha ma neno yenye uzima uliyo ya sikia kwangu, katika imani na upendo ulio katika Kristo Yesu".*

Kama vile tunatoka kuitaja, kazi ya Mwalimu imeungwa sana kwa ile ya Mtume na ya Nabii. Mwalimu hana kazi ya nabii ambayo ni ya kuonyesha sehemu ya unabii na ya historia ya wokovu, bali amepewa kueleza kwa urefu yale yaliyo funuliwa na Mungu kwa huduma ya kinabii na kuyafundisha kwa Kanisa . Mwalimu anachukua sawa sawa hali zote za mafundisho yaki Biblia ambayo yanalihusu Kanisa.

Kazi ya Mwinjilisti inajulikana vizuri na sisi, bali, tutamchukua mwinjilisti Filipo, wa Matendo 8, ili atusaidie kuwa mfano. Muinjilisti ni mtumishi wa Mungu anaye jaa Roho Mtakatifu, anayetangaza injili ya Yesu Kristo kwa nguvu, na ambaye kazi imethbitishwa kwa namna ya kipekee kwa alama, miujiza na uponyaji wa wangojwa.

Kama zile huduma nyingine inne, ile ya Mchungaji haitiliwe mipaka tu kwa Kanisa la mahali, bali ina husu Kanisa lote la BWANA. Mchungaji anabeba daraka la afia njema ya Kanisa. Mchungaji aliwekwa na Mungu anajua ni chakula gani cha kiroho Yule "Mchungaji Mwema" alitangulia kuangiza kwa ajili ya kondoo zake.

## KUWEKWA KWA WAZEE

Katika Kanisa la BWANA, Wazee hawa wekwi kwa uchaguzi wa wengi (ni kusema kwa kura), lakini na mitume, ao na watumishi wa mungu walio tajwa na wao. Paulo na Barnaba ni mfano mzuri wa hayo. Tunasoma katika Matendo 14:23: *"Na walipokwisha kuwachagulia wazee katika kila Kanisa, na kuomba pamoja na kufunga, wakawaweka katika mikono ya BWANA waliyemwamini"*.

Katika Tito 1:5 Paulo anandika: *"Kwa sababu hii nalikuancha Krete, ili uyatengeneze yalio punguka na kuweka wazee katika kila mji kama vile nilivyokuamuru"*.

Maaskofu wanaofanya pia nisehemu ya wazee, kwa maana wako, kama vile matafsiri mengi yana ligeuza, waangalizi wa Kanisa. Hivi neno hili halina maana wanayo lipatiya mara kwa mara leo; Askofu ni mwaangalizi, ao Msimamizi katika kusanyiko la mahali, na ni mmoja wa Wazee. Yule anaye waza kwamba kuelewa kwa sasa kwa tamshi la askofu ni sawa, na akumbuke kila mara kwamba, katika Kanisa la Filipi, mulikuwamo Maaskofu wengi. Tunasoma katika Wafilipi 1:1: *"Paulo na Timoteo, watumishi wa Yesu Kristo kwa wa-*

*takatifu katika Yesu-Kristo walio Filipi kwa ma Askofu na kwa mashemasi..”*

Tunaona hivi kwamba katika Kanisa la mahali, mulikuwamo ma Askofu wengi.

Maaskofu hawa walikua wazee wa Kanisa, katika 1 Timoteo 3, tunasoma haya: “*Kama mtu akitamani kazi ya askofu anatamani kazi njema”*.

Tangu shahiri ya 2, tunaonyeshwa nguvu na uwezo vinavyo hitajika kwa mzee. Anapashwa kuwa bila lawama na wenye kuongoza wema nyumba yake mwenyewe. Hapashwi kua mwamini mupya na awe mwenyi kushudiwa vema na watu wa inje, inafaa awe mwenye kuheshimika, mwenye kiasi katika mwenendo wake, mkaribishaji na anaye jua kufundisha kama vile mwalimu aliye wekwa na mungu kwa ajili ya Kanisa la mahali, na wanapashwa kuwa na uwezo wa kulioyesha mafundisho ya Biblia.

Katika 1 Wathesalonike 5:12-13 Paulo anaandika: “*Lakini ndungu, tunataka muwatambue wale wanaojitabisha kwa ajili yenu, na kuwa simamia ninyi katika BWANA na kuwaonyeni. Mkawastahi sana katika upendo, kwa ajili ya kazi zao. Iweni na amani ninyi kwa ninyi”*. Ndiyo msimamo sawa na walazima katika Kanisa la mahali.

Hali wezi tukupumuzisha matumaini yake juu ya mitume, manabii, wachungaji, waalimu na wainjilisti, lakini linapashwa pia kuwa na matumaini tele katika wazee na wachungaji wa kanisa. Ni hivi tu ndivyo amani na Baraka vina dhaminiwa katika Kanisa.

Katika 1 Timoteo. 5:17, imeandikwa hivi: “*Wazee watawalao vema nawahesabiwe kustihili heshima maradufu, hasa wao wajitaabishao kwa kuhutubu na kufundisha.”* Wazee watimize kazi yao kwa furaha.Ni hivi tu ndivyo wataweza kufanya kazi yao yakuhubiri na ya kufudisha pamoja na kujitoa kabisa. Ni kwa kweli tu kuhusu wazee ndio Mungu aliagiza ulinzi wa kipekee kanisa, Wakati anaposema kwa njia ya Paulo kwenye shahiri 19: *“Usikubali mashitaka juu ya mzee ila kwa vinywa vya mashaidi wawili ao watatu”*.

Mnajua ya kwamba kila mara watu wanapataka kwa urahisi kitu fulani chakusema juu ya wale ambao mungu aliweka na ambao anowatumia kwa ajili ya kubarikiwa kwa Kanisa.Mutu hange lipashwa kupokea neno mbaya juu ya mzee, isipokua kwamba amelisikia toka katika vinya vya mashahidi wa tatu ambao hawakupata-

na kabisa ile haina thamani yoyote, ikiwa watu watatu wamepatana kwa kuleta shitaka inafaa wawe mashahidi watatu wasio patina, ambao hawa kuonana mbele kuhusu jambo lile. Vizuri zaidi ingelikuwa kwamba kanuni hii ishiikwe na jumla yote ya shirika, hivi kuteta yote ya mitaani itakuwa imemalizika. Nina washauri kwamba ikiwa unaletewa shitaka juu ya ndungu ao juu ya dada, usilipokee tu isipokua mbele ya hawa. Mtu hangeli pashwa kuingia katika mazungumuzo kuhusu jambo lile bila kwanza kumupatia mapema mshitakiwa uwezo wa kujitetea.

Katika 1 Timoteo 4:13, Paulo anaandika: *"Hata nitakapo kuja ufanye bidii katika kusoma na kuonya na kufundisha"*.

Kisha anaonya mwenzake wa kazi kuzoeza karama alio ipekea toka kwa Mungu. Katika yaliyomo inaonekana kama Timoteo alipokea zawadi hii kwa kuwekewa mikono ya Wazee. Imeandikwa kwenye shahiri la 14: *"Usiache kuitumia karama iliyomo ndani yako, uliyopewa kwa unabii na kuwekewa mikono ya wazee. Uyatafakari hayo; ukae katika hayo; ili kuendelea kwako kuwe dhahiri kwa watu wote"*. Kwa kumaliza anapana onyo, hili lisilo na mzaha: *"… jitunze nafsi yako, na mafundisho yako, dumu katika mambo hayo …"*

Paulo alitia thamani kubwa kwamba wenzake wa kazi wasimamie kwenye mafundisho yale yale aliyopokea kwa BWANA. Wazee wakiisha kuwekwa na mitume walio anza lile shirika, wanabeba madaraka mbele ya Mungu ya kuendelea kupana lile fundisho bila kosa. Kazi yao na madaraka yao ni kubwa zaidi ginsi watu wasivyozania kwa kawaida. Wakati wa safari moja ya Paulo, aliitisha wazee wa Kanisa. Tunakuta maelezo kuhusu hayo katika Matendo 20:17: *"Toka Mileto, Paulo akatuma watu kwenda Efeso, akwaita wazee wa Kanisa"*. Paulo hakualikaka kamwe mitume, manabii na waalimu, lakini aliwaitisha kwake wazee wa Kanisa la Efeso.

Tunaweza soma sura yote ili kuona ni kwa namna gani alisema na wazee, lakini tuta taja tu shahiri ya 27, ambapo tunaambiwaa: *"Kwa maana sikujiepusha na kuwahubiri kusudi lote la Mungu, jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho mtajatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpaka kulilisha Kanisa lake Mungu, alilonunua kwa damu yake mwenyewe…"*

Tambueni ya kwamba pale ku shahili ya 17, wandungu wanaitwa wazee, lakini kushahiri ya 28, wanaitwa pia maaskofu (waangalizi). Ni yamuhimu sana kutambua ya kwamba wazee wa kanisa hawa-

changuliwi kwa kura ya kanisa, lakini kwamba waliiwekwa vizuri na kazi kama vile waagalizi na Roho Mtakatifu. Wazee wana pia kazi ya kuombea wagonjwa walio sehemu ya Kanisa, wakati muinjilisti kama vile Filipo kule Samaria anaweza kuomba juu ya wote wanao kuja mkutanoni. Imeandikwa katika Yakobo 5:14:

*"Mtu wa kwenu amekuwa hawezi? Na awaite wazee wa Kanisa nao wamwombee, na kumpaka mafuta kwa jina la BWANA, Na kule kuomba kwa imani kutamwokoa ngonjwa Yule na BWANA atamwinua hata ikiwa amefanya dhambi, atasamehewa".*

Tunaweza kutosha katika maneno haya, kama vile tayari tumekwisha kuonyesha pale juu sana kwamba waamini wa shiriki moja siyo kazi yao kuweka matumaini yao kuhusu jambo hili kwa muinjilisti anaye pita lakini kwamba wanapashwa kuyapatia wazee wa Kanisa la mahali walio tayari kila mara kuomba pamoja na wagonjwa. Inglikuwa ya kushauri ya kwamba kila motto wa mungu asome mara tena kwa makini katika maombi kila shahiri la Biblia linayosema kuhusu jambo hili ili tupate mazoezi, upya katika Kanisa la Mungu aliye hai matokeo yaliyo barikiwa ambayo tunangojea kwa hamu kubwa tangu muda murefu.

Imeandikwa katika Waebrania 13.17: *"Watiini wenye kuwaongoza, na kunyenyekea; maana wao wanakesha kwa ajili ya Roho zenu, kama watu watakao toa hesabu"*. Petro anaandika katika 1 Petro 5.1: *"Nawasihi wazee walio kwenu mimi niliye mzee mwenzi wao na shahidi wa mateso ya kristo, na mshirika wa utukufu utakao funuliwa baadaye, lichungeni kundi la Mungu lililo kwenu, na kulimamia, siku kwa kulazimishwa, bali kwa hiari kama Mungu atakavyo, si kutaka fedha ya aibu, bali kwa moyo. Wala si kama wajifanyao ma bwana juu ya mitaa yao, bali kwa kujifanya vielelezo kwa lile kundi. Na mchungaji mkuu atakapo dhihirishwa mtaipokea taji ya utukufu isiyo kauka"*.

Petro akiwa mtume, alikua akijichukua pia kua msimamizi wa kanisa la mahali, sawa sawa na wazee, kwa maana kanisa linaundwa na makusanyiko yote ya mahali. Yote yanayo tokeya katika Kanisa la Mungu aliye hai, iwe kwa njia ya manabii, mitume, wachungaji, waalimu, wainjilisti ao wazee na maaskofu, yote yanatimia kwa ushiraka wa kiungu pamoja na kichwa Yesu-Kristo, na katika uhusiano wa moja kwa wengine.

Nina tambua vema katika dhamiri yangu ya kwamba somo hii imezungumuziwa kwa ufupi, lakini ninayo nataka kwamba kwa yale, kila mmoja awe amesisimuliwa ili kujiigiza zaidi sana katika kilindi cha somo hii. Tusimame imara kwa jambo ambalo ni kwamba: Kanisa la Yesu Kristo siyo matengenezo ya kibinadamu ao kanuni ya imani ambamo wanaweza kuingia wanageuka kuwa viungo vya jamii ya kiulimwengu. Hapana! Ni kitu kilicho wekwa na Mungu-mwili wenye viungo hai. Kila mwanamemba wa Kanisa amezaliwa upya kwa Roho wa Mungu na amejazwa na Roho, ili awekwe chini ya uongozi wa Roho. Kanisa la BWANA halijui hata “kiungo kimoja kisicho kuwa na kazi”.

Akitendwa kwa upande wa Mungu

Ewald Frank

Bro. Frank

Ikiwa unapendezwa kupokea vitabu vyetu, waweza kutuandikia kupitia anwani ifwatayo:


Kituo cha Misheni

Sanduku la Posta 100707

47707 Krefeld

Ujerumani


Waweza kuingia kwenye mtandao wakati wa mikutano yetu ya wikendi ya kwanza ya mwezi. Siku ya Jumamosi Jioni pa saa 19:30 h (Saa ya kati ya Ulaya), Jumapili asubuhi pa saa 10:00 h. Mikutano ya weza kusikilikana katika Lugha 13 tofauti duniani pote.

Pokeeni sehemu kwa yale ambayo Mungu anayo yafanya sasa kulingana na mpango wake wa okovu!


Ukurasa wa vuti: http://www.freie-volksmission.de

Barua pepe : volksmission@gmx.de

Fax: +49-2151/951293

or

www.misia.sk

gospel2nations@misia.sk

Phone: +256 786 892 319/(0)704 721 499, (0)775 283 810



Na Mwandishi na Mchapishaji E.Frank